# Ni Wakati wa Mambo Makubwa,
# Inuka Uangaze!

## Mpango Mkakati wa Kanisa la
## Pentecostal Assemblies of God (Tanzania)
***2021-2031***

© Mei 2021

## MUHTASARI KUTOKA KWA ASKOFU MKUU

Mungu wetu hafanyi jambo lolote bila kuwa na Mpango. Kwa mfano, ukombozi wa mwanadamu haukuwa jambo la kushtukiza bali lilikuwa katika Mpango wa Mungu wa muda mrefu sana (Mwanzo 3:15). Hivyo, twaweza kusema ni tabia ya Mungu kufanya mambo kimkakati. Yatupasa basi sisi watumishi wake tuwe na hii tabia ya kujipangia mambo yetu ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwani kwa kufanya hivyo tunaiakisi tabia ya Mungu wetu.

Ni dhahiri kuwa nyakati na majira vimebadilika. Mpango Mkakati huu unaakisi mabadiliko ya nyakati zetu na kutufanya tusibaki nyuma kwa kuendelea kutumia mbinu za zamani huku tukitegemea matokeo makubwa. Katika kuuandaa Mpango Mkakati huu, tathmini ya kina ilifanyika kwa kuangalia Nguvu zetu, Madhaifu yetu, Fursa zilizopo pamoja na Vitisho. Lakini pia, tathmini ya jumla ya hali ya nchi Kisiasa, Kiuchumi, Kisheria, Kiteknolojia na Kimazingira ilifanywa ili kutusaidia kuweka Malengo na Mikakati inayoitikia muktadha wa sasa wa Kanisa. Huu ulikuwa ni mchakato shirikishi na ulifanyika kwa hatua mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye Sura ya tano ya Mpango Mkakati huu. Baada ya hatua zote hizo, Mpango Mkakati huu ulipitiwa na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu ya PAG (T), ikifuatiwa na warsha ya siku mbili kwa Baraza la Waangalizi kabla ya kuzinduliwa rasmi mnamo tarehe 14 Mei, 2021. Hivyo, basi Mpango Mkakati huu utakuwa ndio mwongozo wa utendaji wa kazi ya Mungu katika Kanisa letu la PAG (T) kwa miaka kumi, yaani kuanzia 2021 mpaka 2031. Tunayo maeneo makuu ya Kimkakati kumi (10) yenye Malengo Mkakati kumi na tatu (13). Makanisa ya mahali, maasembli, wilaya, majimbo, Halmshauri Kuu, pamoja na idara zote zinahimizwa kutekeleza Mpango Mkakati huu katika Mipango kazi yao.

Kipekee namshukuru Mungu sana na nimejawa na furaha tele kwa hatua hii tuliyoifikia ya kuwa na Mpango Mkakati huu. Ni maombi yangu kuwa Mungu atatukuzwa kwa kazi njema tutakayomfanyia katika kumvunia mavuno na kumwandalia watenda kazi katika shamba lake. Kwa kufanya hivyo tutakuwa pia tunatimiza Dira, Dhamira na Malengo yetu kama dhehebu. Hakika, huu

***Ni wakati wa mambo makubwa, inuka uangaze!***

Ni Mtumishi Mwenzenu,



Rev. Dkt. Daniel Awet Alley

ASKOFU MKUU
PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD (TANZANIA)

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BoQ | Bill of Quantities |
| CA | Christ Ambassadors |
| CCP | Child Care Plus |
| CCT | Christian Council of Tanzania |
| CIT | Compassion International Tanzania |
| COVID-19 | Corona Virus Diseases – 2019 |
| CPCT | Council of Pentecostal Churches in Tanzania |
| CRS | Catholic Relief Services |
| DPC | Dar es Salaam Pentecostal Church |
| EAGT | Evangelist Assemblies of God Tanzania |
| EKK | Eneo Kuu la Kimkakati |
| FGM | Female Genital Mutilation |
| FPCT | Free Pentecostal Church of Tanzania |
| GDP | Gross Domestic Product |
| HIV | Human Immunodeficiency Virus |
| HQ | Head Quarter |
| ICT | Information, Communication, and Technology |
| ILI | International Leadership Institute |
| KSA | Key Strategic Area |
| LCD | Liquid-Crystal Display |
| LM | Lengo Mkakati |
| MBB | Muslim Background Believer |
| MCC | Mwanza Christian College |
| MKUKUTA | Mpango wa Kuondoa Umasikini na Kukuza Uchumi Tanzania (Swahili version of NSGRP) |
| NACTE | National Council of Technical Education |
| NGO | Non-Governmental Organization |
| NSGR | National Strategy for Growth and Reduction of |

| | |
|---|---|
| P | Poverty |
| ODK | Open Data Kit |
| PAG (T) | Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) |
| PAGBC | Pentecostal Assemblies of God Bible College |
| PAOC | Pentecostal Assemblies of Canada |
| PCN | Pastors' Children Network |
| PESTEL | Political, Economic, Social, Technological, Environmental, and Legal |
| PPN | PAG (T) Professionals' Network |
| RBS | Regional Bible School |
| ROPE | Rites of Passage Experience |
| SACCOS | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SDA | Seventh Day Adventist |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| STEP | Students' Transformational Empowerment Program |
| SWOT | Strengths, Weaknesses, Opportunities, and Threats |
| TAG | Tanzania Assemblies of God |
| TCRA | Tanzania Communications Regulatory Authority |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TDV | Tanzania's Development Vision |
| TEC | Tanzania Episcopal Council |
| TEHAMA | Teknolojia, Habari na Mawasiliano |
| ToR | Terms of Reference |
| VBS | Vacation Bible School |
| VOH | Village of Hope |
| WWK | Wanawake Watumishi wa Kristo |

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| **MUHTASARI KUTOKA KWA ASKOFU MKUU** | | i |
| **ORODHA YA VIFUPISHO** | | iii |
| **YALIYOMO** | | V |
| **SURA YA KWANZA** | | 1 |
| **MAELEZO YA UTANGULIZI** | | 1 |
| | | |
| **SURA YA PILI** | | 5 |
| **MFUMO WA UONGOZI WA PAG (T)** | | 5 |
| 2.1 | Mkutano Mkuu | 5 |
| 2.2 | Baraza la Waangalizi | 5 |
| 2.3 | Halmashauri Kuu | 5 |
| 2.4 | Kamati Tendaji | 6 |
| 2.5 | Idara | 6 |
| 2.6 | Ngazi ya Jimbo | 6 |
| 2.7 | Ngazi ya Wilaya | 7 |
| 2.8 | Assembli na Kanisa la Mahali | 7 |
| | | |
| **SURA YA TATU** | | 8 |
| **MWELEKEO WA KIMKAKATI WA PAG (T)** | | 8 |
| 3.1 | Dira ya PAG (T) | 8 |
| 3.2 | Dhima ya PAG (T) | 8 |
| 3.3 | Maadili ya Msingi ya PAG (T) | 8 |
| 3.4 | Kauli Mbiu ya PAG (T) | 10 |
| 3.5 | Tamko la Imani ya PAG (T). | 11 |
| 3.6 | Malengo (Shabaha) ya PAG (T) | 12 |
| | | |
| **SURA YA NNE** | | 14 |
| **MSINGI WA MPANGO MKAKATI HUU** | | 14 |
| 4.1 | Msingi wa Kibiblia katika Mpango Mkakati | 14 |
| 4.2 | Kupanga kwa Imani | 15 |
| 4.3 | Faida za Kupanga Kimkakati | 16 |
| | | |
| **SURA YA TANO** | | 19 |
| **MCHAKATO WA KUANDAA MPANGO MKAKATI HUU** | | 19 |
| 5.1 | Toleo la Kwanza | 19 |

5.2 Toleo la Pili 19
5.3 Warsha ya Mpango Mkakati 20
5.4 Timu ya Mpango Mkakati 20

**SURA YA SITA** 21
**UCHAMBUZI WA KIMAZINGIRA** 21
6.1 Uchambuzi wa SWOT: Ndani 21
6.2 Uchambuzi wa PESTEL: Nje 26

**SURA YA SABA** 30
**MAENEO MAKUU YA KIMKAKATI NA MALENGO MKAKATI** 30

**SURA YA NANE** 34
**CHATI YA UTEKELEZAJI** 34

**SURA YA TISA** 156
**UFUATILIAJI NA TATHIMINI** 156

**VIAMBATANISHO** 158
1. Washiriki wa Warsha ya Mpango Mkakati– VETA Dodoma – Sept 21-26, 2020 158
2. Ratiba ya Warsha ya Mpango Mkakati wa PAG (T) - Sept 21-26, 2020 @ Veta Dodoma 159
3. Timu ya Mpango Mkakati: Awamu ya Pili na ya Tatu 170
4. Ratiba ya Warsha ya Mpango Mkakati wa PAG (T) –
5. Chati ya Uongozi wa PAG (T) 174
Zanzibar, Nov 9 – 14, 2020 170
6. Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa PAG (T): Kalenda ya Mwaka – Mfano 175
7. Matarajio ya Washiriki wa Warsha ya VETA – Dodoma 179
8. Hofu na Majibu Yake 179
9. Agano la Kiongozi wa PAG (T) 181
10. Sehemu ya Hotuba ya Askofu Mkuu Kwenye Mkutano Mkuu Septemba 29, 2019 183

## SURA YA KWANZA

## MAELEZO YA UTANGULIZI

The Pentecostal Assemblies of God (Tanzania), kwa kifupi PAG (T), ilianzishwa na wamishenari kutoka Kanada chini ya Pentecostal Assemblies of Canada (PAOC), tawi la Kijerumani, mapema mwanzoni mwa miaka ya 1950. Wamishenari hawa wa kwanza waliwasili nchini Tanzania wakitokea Kenya kupitia mpaka wa mkoa wa Mara na kuanzisha kituo cha umisheni pale Nyasirori, Butiama ambayo sasa ni wilaya. Kabla ya kuanzishwa kwa kituo cha umisheni Nyasirori, wainjilisti na wachungaji wa PAG (T) kutoka iliyokuwa Tanganyika (sasa Tanzania Bara), walipata mafunzo ya kiutumishi kutoka Shule ya Biblia ya Nyang'ori, nchini Kenya, iliyoanzishwa miaka ya 1950[1], na waliporejea nchini walipanda makanisa ya mahali hasa mkoani Mara. Kadri kazi ya umisheni ilivyokuwa ikikua Tanzania Bara, wamishenari wa PAOC walianzisha Shule ya Biblia katika maeneo ya Nyasirori na ndipo walianza kufundisha na kuwaandaa viongozi wa kitaifa na maeneo ya mahali husika kwa ajili ya kazi ya huduma.

Ni muhimu kukumbuka kuwa waanzilishi wa kwanza wa huduma ya PAG (T) walijitoa maisha yao kwa ajili ya kuupanua ufalme wa Mungu Tanganyika. Nyakati hizo baadhi ya wamishenari walipoteza uhai wao kutokana na magonjwa kama vile malaria na kuzikwa Tanganyika. Baadhi ya makaburi yao yapo hadi leo katika maeneo ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoa wa Singida. Bahati mbaya, kutokana na udhaifu katika

[1] Hata hivyo, historia kamili inaonyesha kuwa wamishonari wa kwanza kabisa kutoka PAOC waliingia Tanganyika miaka ya 1910, lakini kazi haikusimama. Angalia kiambatanisho cha 10 kwa maelezo ya zaidi ya historia ya PAG (T) kama yalivyotolewa katika sehemu ya hotuba ya Askofu Mkuu wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2019.

utunzaji kumbukumbu, haijawezekana kujua idadi yao waliopoteza uhai wao na majina yao halisi.

Ilikuwa mnamo mwaka 1967, PAG (T) ilipopata usajili wa muda kutoka serikali ya Tanzania, na mwaka huo wakamchagua Askofu Mkuu wa kwanza na viongozi wengine wa kitaifa. Kabla ya hapo PAG (T) ilikuwa sehemu ya makanisa ya Pentecostal Assemblies of God East Africa (PAGEA). PAG (T) ilipokea cheti cha usajili kamili namba SO. 6510 mnamo 1987.

Tangu kuanzishwa kwake, PAG (T) iliwekeza zaidi katika kuandaa viongozi, hivyo kupelekea kuanzisha Shule za Biblia. Kama ilivyosemwa hapo juu, katika mwaka 1967, wamishenari wa PAOC walianzisha Shule ya Biblia kule Nyasirori, mkoani Mara chini ya uongozi wa Rev. Paul Schellert. Mafunzo yalitolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa kipindi cha wiki mbili kila mwaka kwa miaka mitano. Mahafali ya kwanza kabisa yalifanyika Nyasirori mwaka 1971 na katika mwaka 1976 shule ilihamishwa kutoka Nyasirori kwenda Mwanza. Mnamo 1978 chini ya uongozi wa mmishenari wa PAOC Rev. John Haug jina la shule lilibadilishwa kutoka Shule ya Biblia Mwanza na kuwa Chuo cha Biblia Mwanza, japokuwa lugha ya kufundishia iliendelea kuwa Kiswahili. Wanafunzi walisoma kwa wiki nane kila mwaka kwa miaka minne. Mwaka 1988, chini ya uongozi wa mmishenari wa PAOC, Rev. Leonard Rutten, chuo kilianzisha programu ya stashahada (diploma) iliyofundishwa kwa lugha ya Kiingereza, na chuo kubadili jina na kuitwa Pentecostal Assemblies of God Bible College (PAGBC). Mwaka 2005, PAGBC ilianzisha programu ya shahada ya Biblia na Theolojia kwa ushirika wenza na Chuo Kikuu cha Pan Africa Christian cha Nairobi.

Zaidi ya chuo cha Biblia cha Mwanza, wamishenari wa PAOC, chini ya uongozi wa Rev. Gordon Wiebe, ulianzisha mfumo wenye mafanikio wa kuendeleza na kupatia mafunzo viongozi wa Shule za Biblia za Mikoa, Regional Bible Schools (RBS). Hivi ni vituo vya mafundisho ya kiutumishi vilivyojengwa katika mikoa 13 hivi ili kuwaandaa washirika wa PAG (T) wenye wito wa Mungu maishani mwao katika mazingira waliyopo, wakitumia lugha ya Kiswahili, kwa kazi ya kichungaji. Wengi wa wachungaji wa PAG (T) ni wahitimu wa shule hizi. Shule za RBS zimeendelea kuwa uti wa mgongo wa PAG (T) katika kufundisha na kuandaa watumishi wa kanisa.

Ijapokuwa ni kweli kuwa PAG (T) inapatikana zaidi maeneo ya vijijini, ni muhimu kutambua kuwa, hata hivyo, wamishenari wa PAOC waliwekeza zaidi vile vile mijini. Makanisa mengi ya mijini, kama vile Musoma, Mwanza, Bukoba, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Singida, Morogoro, yalianzishwa na wamishenari waliohakikisha pia wananunua ardhi ya kutosha kujenga majengo ya makanisa na shughuli nyingine, ikiwa ni pamoja na RBS.

Kwa miaka mingi, PAG (T) imekua na kusambaa karibu katika mikoa yote ya Tanzania. Wakati mkakati huu unaandikwa kulikuwa na makanisa 1,717, washirika 56,794, watoto 48,652, wachungaji wasimikwa 702, wachungaji wasiosimikwa 962, wachungaji wenye mafunzo ya ngazi ya cheti (RBS) 721, wachungaji wenye elimu ngazi ya stashahada 83, wachungaji wenye elimu ngazi ya shahada 41, wachungaji wenye elimu ngazi ya shahada ya uzamili 9, na wachungaji wenye elimu ngazi ya shahada ya uzamivu 2.

Kwa mujibu wa historia hii, ni dhahiri kuwa PAG (T) ilikazania zaidi maendeleo ya kiroho hivyo kupelekea pengo katika kushuguhulikia mahitaji ya msingi ya kibinadamu kwa ujumla wake. Matokeo yake, kwa zaidi ya miaka hamsini ya uhai wake,

PAG (T) inamiliki shule za awali 28, shule za msingi 0, shule ya sekondari 1, vyuo vya kati (tofauti na vitoavyo elimu ya Biblia vilivyotajwa juu) 0, vyuo vya ufundi 0, vyuo vikuu 0, miradi au programu za kiuchumi/kijamii 0. Hata hivyo, kwa ushirikiano na Compassion International Tanzania, PAG (T) ina vituo 17 (katika makanisa ya mahali), vinavyohudumia watoto 3,942.

Mpango Mkakati huu unalenga katika kutoa mwelekeo wa hili pengo (la ukosefu wa programu za maendeleo ya kiuchumi na kijamii) kwa uelewa kuwa Injili inapaswa kugusa mahitaji yote kiukamilifu; kiroho, kiuchumi, kijamii na kimwili. Agizo Kuu na Amri Kuu vinapaswa kutimizwa kwa pamoja, zaidi katika kushughulikia kujumuisha mahitaji yote ya kiroho ya kimwili kwa pamoja, na huo ndio msukumo mkuu wa Mpango Mkakati huu.

## SURA YA PILI

## MFUMO WA UONGOZI WA PAG (T)

2.1 Mkutano Mkuu

Mkutano Mkuu ndio wenye mamlaka ya mwisho katika PAG (T) na hukutana mara moja kila baada ya miaka mitano. Kwa mujibu wa katiba, mkutano huu unajumuisha wachungaji wote wasimikwa na wasio simikwa pamoja na wenzi wao, walimu wa shule na Chuo cha Biblia pamoja na wenzi wao, wakurugenzi wote wa idara kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa, na wamishenari wakazi. Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, unawajibika kuchagua viongozi wa kitaifa ambao ni Askofu Mkuu na makamu wake, Katibu Mkuu na naibu wake, wajumbe wawili, na wakurugenzi mbalimbali wa idara ngazi ya kitaifa.

2.2 Baraza la Waangalizi

Baraza la Waangalizi ni ngazi ya pili katika mfumo wa uongozi wa PAG (T). Baraza hili linaundwa na wajumbe wote wa kamati ya Halmashauri Kuu, Waangalizi wote wa wilaya, wajumbe wa Baraza la Wadhamini, na Maaskofu wakuu wastaafu. Chombo hiki hupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Halmshauri Kuu na kupendekeza njia za kuboresha huduma za PAG (T). Wakati wa Uchaguzi Mkuu, chombo hiki hupendekeza majina ya wagombea kwa Mkutano Mkuu wa uchaguzi kwa ajili ya kupigiwa kura. Baraza hili pia linahusika na kujadili na kukubaliana juu ya mabadiliko ya Katiba yatakayopelekwa Mkutano Mkuu kupitishwa.

2.3 Halmashauri Kuu

Halmashauri Kuu huundwa na viongozi wote wa kitaifa, Maaskofu wa majimbo, Wajumbe wawili na Wakurugenzi wa Idara kitaifa. Halmashauri kuu hutumika kama chombo cha usimamizi ndani ya PAG (T), ambayo hukutana mara tatu kwa

mwaka na hupokea na kujadili mambo mbali mbali ya kidhehebu, pamoja na taarifa kutoka maaskofu wa majimbo na kwa wakurugenzi wa idara za kitaifa. Chombo hiki pia ndicho husimamia mchakato wa maombi na kutafuta kibali cha kazi kwa wamishenari wa kigeni ambao wangependa kufanya kazi na PAG (T). Halmashauri Kuu imepewa mamlaka kuunda idara zingine uhitaji unapojitokeza.

### 2.4 Kamati Tendaji

Halmashauri Kuu pia imekasimisha sehemu za shughuli zake kwa Kamati Tendaji ambayo inaundwa na Askofu Mkuu, katibu mkuu, na Makamu wao. Kamati hii ni chombo cha utekelezaji ambacho hushughulikia majukumu ya siku kwa siku ya kiofisi na kushughulikia mambo ya dharura na maamuzi yake huthibitishwa na Halmahsauri Kuu.

### 2.5 Idara

Katiba ya PAG (T) inataja idara za kitaifa sita, ambazo ni pamoja na idara ya Wanawake, Vijana, Umisheni na Uinjilisti, elimu na Mafunzo, Wanaume, na Watoto. Ibara ya 36 inataja idara mbili zinazoshabihiana ambazo ni huduma za hifadhi ya jamii na huduma za maendeleo. Idara hizi zote zina wakurugenzi ambao wanawajibika kwa Askofu Mkuu na kwa Halmashauri Kuu. Wakati Mkakati huu unaandikwa, idara tatu mpya zilikuwa zimemalizika kuundwa na wakurugenzi wake kuteuliwa. Idara hizo mpya: idara ya Elimu na Mafunzo, Umisheni na Uinjilisti, na Maendeleo ya jamii. Idara ya Watoto na wanaume bado hazijapata wakurugenzi.

### 2.6 Ngazi ya Jimbo

Ngazi inayofuata katika mfumo wa utawala wa PAG (T) ni Majimbo. Majimbo mengi yapo katika mipaka ya mikoa sawa na serikali isipokuwa machache tu. Wakati wa kuandika Mpango Mkakati huu, PAG (T) ilikuwa na Majimbo kumi na sita ambayo ni: Jimbo la Arusha (Arusha na Kilimanjaro), Jimbo la Dar es Salaam (Dar es Salaam, Lindi, Pwani na Zanzibar ), Jimbo la

Dodoma, Jimbo la Geita, Jimbo la Iringa (Iringa, Njombe na Ruvuma), Jimbo la Kagera, Jimbo la Kigoma, Jimbo la Manyara (Manyara na Singida), Jimbo la Mara, Jimbo la Mbeya (Mbeya, Rukwa, na Songwe), Jimbo la Morogoro, Jimbo la Mwanza, Jimbo la Shinyanga, Jimbo la Simiyu, Jimbo la Tabora, na Jimbo la Tanga. Majimbo haya yote yanaongozwa na maaskofu ambao pia huchaguliwa kila baada ya miaka mitano. Maaskofu hawa wamekasimishwa madaraka ya kusimamia wilaya zote katika majimbo yao husika ikiwa ni pamoja kuwa wenyeviti wa mikutano yote ya kijimbo na mkutano mkuu wa jimbo.

## 2.7 Ngazi ya Wilaya

Baada ya jimbo, inafuata ngazi ya wilaya. Wakati wa kuandika mkakati huu, PAG (T) ilikuwa inafanya kazi katika wilaya hamsini na saba (57) kati ya wilaya mia moja themanini na saba (187) ya Tanzania Bara na Visiwani. Hii inaonyesha kuwa PAG (T) bado inayo kazi kubwa ya kupanda makanisa imara katika wilaya zilizosalia. Kiongozi mkuu katika wilaya ni Mwangalizi. Kiongozi wa nafasi hii pia huchaguliwa kila baada ya miaka mitano na yeye ni msimamizi wa Asembli zote katika Wilaya husika.

## 2.8 Assembli na Kanisa la Mahali

Msingi wa uwepo wa PAG (T) ni Assembli na Kanisa la mahali pamoja. Assembli huundwa na makanisa kadhaa, au matawi. Sifa ya msingi ya kuwa Assembli ni kuwa na mchungaji msimikwa. Kanisa la mahali (tawi) kwa kawaida huanzishwa au kuasiliwa na Assembli na hivyo kuwa chini ya uangalizi wa assembli husika. Si lazima kwa kanisa la mahali (tawi) kuwa na mchungaji aliyesimikwa, lakini halizuiliwi kuwa naye. Kwa kawaida, assembli itamchagua Mwenyekiti, katibu, na viongozi wa Idara wa Assembli kutokana na makanisa yaliyo chini yake. Hata hivyo, kwa maeneo ya mijini mfumo wa Assembli hauna mafanikio na hivyo kila kanisa la mahali hujiendesha kama Assembli inayojitegemea.

# SURA YA TATU

## MWELEKEO WA KIMKAKATI WA PAG (T)

3.1 Dira ya PAG (T)
Dira ya Kanisa la PAG (T) ni kuwa Kanisa linalombadilisha kila mtu kwa Injili ya Kristo kiroho, kimwili na katika nafsi yake.

3.2 Dhima ya PAG (T)
Dhima ya PAG (T) ni kumwabudu Mungu katika roho na kweli na kuihubiri Injili katika nguvu za Roho Mtakatifu kwa kila mtu na kila mahali, kuanzisha na kuimarisha makanisa ya mahali yatakayokuwa chumvi na chachu ya mabadiliko kuleta ufalme wa Mungu kwa watu wake na viumbe vyote.

3.3 Maadili ya Msingi ya PAG (T)

a) Ukamilifu
Tunaitikia mahitaji ya jamii kikamilifu kwa kuunganisha uinjilisti na huduma za kijamii. Tunapanda makanisa sambamba na kuanzisha huduma nyingine za jamii ambazo zinamsaidia mwanadamu kiroho, kimwili, kijamii na kiuchumi. Bwana na Mkombozi wetu Yesu Kristo ndiye kielelezo katika huduma hii muhimu (Luka 4:18-19).

b) Hofu ya Mungu
Tumeokolewa kumwabudu Mungu pekee kwa vinywa vyetu, mioyo, nafsi zetu na katika roho na kweli. Tunamtambua Bwana Mungu kama ndiye Mkuu ambaye hana mwanzo wala mwisho. Yeye ni Muumba na sisi tu viumbe wake tuliowekwa huru kutoka utumwa wa dhambi kwa neema yake. Kwa hiyo tunakataa dhambi na kujitahidi kuishi maisha ya kumpendekeza Mungu kuanzia Jumapili hadi Jumapili (Zab. 24:3-10).

c) Heshima
Tumedhamiria kupendana sisi kwa sisi kwa upendo wa undugu.Tunaahidi kuwa watiifu kwa viongozi wetu kama wanavyofuata mfano wa uongozi wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tutaendelea kufuata maelekezo kutoka kwa viongozi kwa utendaji. Tumedhamiria kujaliana sisi kwa sisi kwa heshima kwa sababu watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Tunatafuta kuelewa wanachosema wenzetu kabla ya sisi kueleweka na tunajitahidi kuepuka kadiri iwezekanavyo kuwahukumu ndugu zetu katika Bwana, hasa watumishi wenzetu. (1 Pet. 2:17; Waebr. 13:7-8).

d) Umoja
Tunahamasisha umoja wa mwili wa Kristo kama amri iliyotolewa na Bwana Yesu Kristo. Tunakataa utengano wowote. Viongozi wote wa PAG (T) wanategemea kuwa mabalozi wazuri wa umoja wa Kanisa kwa sababu tunaamini kwamba ili Kanisa libarikiwe inabidi waumini waungane katika agenda ya ki-Mungu ya kuwafanya wanafunzi katika mataifa yote na katika kufanya hivyo kazi ya Mungu itaenea haraka zaidi kuliko kawaida (Zab.133:1-3; Yoh 17:21).

e) Uharaka
Tunaamini kwa dhati kuwa Yesu Kristo anarudi upesi, muda ni mfupi sana, na wajibu wetu ni kuwafikia mataifa yote na kuwafanya kuwa wanafunzi wa Yesu. Hatufumbii macho roho ya ukawaida kwani inadhoofisha kazi ya umisheni. Tunaitikia masuala ya kidhehebu na kanisa la mahali kwa wepesi na kuchukua hatua stahiki haraka sana iwezekanavyo (Mat. 28:18-20; War. 13:11).

f) Uwakili, uwazi na uwajibikaji
Tunaamini kwamba rasilimali zote (binadamu, fedha, vitendea kazi) zimekabidhiwa kwetu na Mungu kwa ajili ya

kukuza Ufalme wake. Kama mawakili wa Mungu, tunaahidi kuwa waaminifu katika namna ya kutumia na kuendeleza watu na rasilimali nyingine, hasa fedha. Tunaona kitu chochote kilichowekwa katika mikono yetu katika mtazamo wa ki-Mungu na tunatumia falsafa ya kutovumilia ubadhilifu wowote wa rasilimali za Mungu - mali na fedha. Tunawajibishana kwa kuweka mifumo yenye uwazi (Mwa. 2:15; Mwa 39:4; Dan 6:1-3; 1Wakor 4:1-2).

g) Mabadiliko

Tunaamini kwamba malengo yote ya ujumbe wa Injili ni mabadiliko ya moyo wa binadamu, mifumo na miundo. Asili ya neno la Kiyunani, mabadiliko, inaeleza mabadiliko katika muundo kutoka hatua moja kwenda nyingine. Mabadiliko ya Kibiblia ni mchakato wa maisha ya muda mrefu ambao unahitaji uvumilivu, neema na kuhubiri Injili ya kweli ya Bwana wetu Yesu Kristo (War 12:2; Wakol.3:5; Waef 4:15).

3.4 Kauli Mbiu ya PAG (T)

**"Ni Wakati wa Mambo Makubwa, Inuka Uangaze."**

Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua - (Yeremia 33:3).

Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia - (Isaya 60:1).

Tunaamini kwamba Mungu wetu ni Mungu wa Mambo Makubwa, hivyo tukimwita, tukiondoka, tukiangaza na kukataa mambo manyonge yaliyo chini ya viwango, utukufu wa Bwana utatuzukia.

3.5 Tamko la Imani ya PAG (T).

Tunaamini:

a) Kwamba kuna Mungu mmoja mwenye enzi ya milele katika Utatu: Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu (Kumb. 6:4; Mk. 12:29; Mt 28:19; 2 Kor. 13:14).

b) Katika uumbaji mkamilifu wa Mungu kwa binadamu, mume na mke, kwa mfano wake, na viumbe vyote, na kwamba kulikuwa na anguko la malaika na mwanadamu ambalo matokeo yake yameleta maumivu na uharibifu na kifo cha kiroho na cha kimwili. (Mwa. 1:1, 26 - 27, 31; 3:1-19; Rum. 3:23).

c) Biblia imevuviwa na Mungu, ni Neno la Mungu lenye mamlaka na lisilokuwa na makosa nayo ndiyo msingi wa imani yetu na mwenendo wa Kikristo (2 Tim 3:15-17; 2 Pet. 1:21).

d) Katika Uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, katika kuzaliwa kwake na bikira huyo ni Mariamu, katika maisha yake yasiyo na dhambi, katika miujiza yake, katika kifo chake badala ya wenye dhambi ambacho kilifanyika upatanisho kati ya mwanadamu na Mungu, na katika ufufuo wake katika mwili na kupaa kwake mbinguni na kukaa mkono wa kuume wa Mungu Baba, na katika kurudi kwake mara ya pili hapa duniani katika nguvu na utukufu ili kuyatawala Mataifa (Mt. 1:18-23; 16:15-16; Mk. 16:19; Mdo. 1:9-11; 2 Kor. 5:17; Kol.1:15).

e) Kwamba njia pekee ya wokovu wa binadamu kutoka dhambini ni kutubu na kuacha dhambi na kumwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa

maisha yake na kwa kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu (Yoh.1:11-13; 3:5-8; Mdo. 2:38; Rum. 10:9; 1Yoh.1:9)

f) Katika kuponywa kwa mwili wa binadamu ambako kumepatikana kwa njia ya kifo kwa kupigwa kwake Yesu Kristo na kifo chake msalabani, na uponyaji huo hupokelewa kwa ombi la imani (Isa. 53:1-5; Mk.16:16 - 18).

g) Katika ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na ushuhuda wa kunena kwa lugha kunakofuatana na Tunda la Roho, kunakopokelewa kwa imani ikiambatana na masharti ya Biblia ya kupokea ubatizo huo (Yoh.7:37; 14:16 -17; 16:12 - 15; Mdo.1:8; 2:1- 4; 10: 44 - 47; 19:2-6).

h) Kanisa ni watu walioitwa na Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kutoka ulimwenguni na kuwekwa wakfu kwa ajili yake, kwa kuzaliwa mara ya pili na kuunganishwa katika mwili wa Kristo, ambaye ni kichwa cha Kanisa. Kazi ya Kanisa ni kumpenda na kumtukuza Mungu na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe na kuishi katika tumaini la ufufuo wa wafu (Mt. 5:13 - 14; Yoh. 15:1, 2; Mdo. 1:8; Efe. 1:7, 22; 4:11-16; 5:23; 2 Kor. 6:6 -18).

3.6 Malengo (Shabaha) ya PAG (T)

a) Kuhubiri Injili kwa kila kiumbe na kufundisha Neno la Mungu ili kuwafanya walioamini kuwa wanafunzi wa Yesu.

b) Kuanzisha na kuimarisha makanisa mijini, vijijini na kila mahali wanakoishi watu; makanisa yanayomtii Kristo na kuieneza Injili yake; na makanisa yenye

uwezo wa kujieneza, kujitegemea na kuihudumia jamii mahali yaliko.

c) Kuweka tayari mafundisho mema ya kikristo kwa washirika wote kwa njia ya vitabu, mafundisho ya shule za Biblia, mikutano ya Injili na semina, mafundisho kwenye radio, runinga yatakayowaimarisha washirika kiroho, kiakili, na kimwili.

d) Kuanzisha taasisi za elimu ili kutimiza malengo ya Kanisa.
e) Kuendesha miradi na Huduma za Jamii.

## SURA YA NNE

## MSINGI WA MPANGO MKAKATI HUU

Kwa mujibu wa Guy S. Saffold,[2] vipengele vifuatavyo vinaonesha msingi wa kibiblia wa kila mchakato wa kuandaa mpango mkakati wowote wa Kikristo, ukiwemo na huu.

4.1 Msingi wa Kibiblia katika Mpango Mkakati

a) Tabia ya Mungu: Ukitazama na kuchunguza uumbaji, ni dhahiri kuwa unaonesha mambo ya ajabu, halisi, utaratibu, na kuonesha mpangilio (Zab. 19:1). "Mungu wetu hafanyi lolote bila mpango au kusudi" (ukurasa 2).

b) Kanuni za Kibiblia za Mpango Mkakati

i) *Unalenga mambo yajayo:* Ukianzia na mambo yaliyopo ya leo, Mpango Mkakati unajikita katika kuangalia fursa zijazo kesho. Mtume Paulo anadhihirisha ukweli huu katika waraka wake kwa Warumi 15:20-25.

ii) *Huzingatia maono:* Maono ni kipengele muhimu katika kuandaa Mpango Mkakati. Katika 1 Mambo ya Nyakati 28, mfalme Daudi alipata maono ya kumjengea Bwana hekalu. Wazo hili lilimjia ikiwa ni matokeo ya kutafakari nafsini mwake juu ya ulinganifu Wa ajabu na wa kuvutia wa makazi yake akilinganisha mahali sanduku la Agano la Mungu lilipokuwa nyumba yake. Kutoridhika katika mambo ya kimungu ndio sehemu ya kuanzia mchakato wa kuandaa Mipango Mkakati

[2] Guy S, Saffold, *Strategic Planning: Leadership Through Vision.* (Nairobi: Evangel Publishing House, 2005), 1-17.

iii) *Husisitiza utekelezaji:* "Utekelezaji bila Mipango ni kukosa shabaha, lakini Mipango bila utekelezaji haizai matunda" (uk. 11). Lengo la kupanga kimkakati ni kuhamasisha kazi (utekelezaji). Nehemia ni mfano mzuri wa mtu wa imani na kazi (utekelezaji). Utekelezaji unaotegemezwa na maombi ya bidii unapaswa kusisitizwa (Nehemia mlango wa 1)

iv) *Hutarajia na kuwa tayari kwa mabadiliko:* Habari ya ndoto ya Farao katika kitabu cha Mwanzo ni mfano wa uhakika. Mambo hayakufanyika kama alivyokuwa amepanga na hivyo kulazimu Yusufu kuongezwa kwenye safu ya utendaji kusimamia mabadiliko(Mwa.41)

v) *Kuwa mwepesi kubadilika inapohitajika:* Sisi kama binadamu, hatuwezi kuelewa kwa usahihi mambo yajayo. Kwa mfano, Mpango wa Mtume Paulo kuitembelea Hispania haukufanikiwa, badala yake aliishia Rumi akiwa mfungwa, jambo ambalo hakuwahi kuliwaza. Wakati mwingine Mungu anaweza kufuta Mipango yetu. Kwa hiyo, ni muhimu kupitia upya mara kwa mara au hata kuachana kabisa na mipango isiyoendana na wakati katika ulimwengu unaobadilika. Tazama Mithali (21:30-31).

## 4.2 Kupanga kwa Imani

Mpango Mkakati unapaswa kufanywa kwa imani yenye kina katika elimu ya Mungu na iliyo hai katika kutembea naye kila siku. Kutembea na Mungu kila siku ni muhimu hutujengea ujasiri kwa Mungu asiyebadilika. Yeye agawaye hekima na maarifa kupambanua katika kufanya maamuzi yetu juu ya mambo yajayo, ambayo hakuna ajuaye ya kesho (Yakobo 1:5). Viongozi wa Kikristo wanapaswa kuweka mipango ipitayo uwezo wao kwa sababu Mungu "awezaye kufanya mambo ya ajabu kuliko yote tuyaombayo au

tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu" (Efe. 3:20).

### 4.3 Faida za Kupanga Kimkakati

Guy S. Saffold[3] anataja faida 7 za kupanga kimkakati. Kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkakati huu, tutaziangalia sita kati ya hizo.

a) *Kuendana na mabadiliko*
Mabadiliko hayaepukiki. Ulimwengu leo unabadilika kwa kasi inayoongezeka. Janga la Korona ni mojawapo wa mifano mingi. Watu wengi husema na kufikiri, "mambo yatatulia" au "hali itarejea kama awali." Ukweli wa mambo ni kuwa kamwe hali huwa haitulii kama mwanzo. Uongozi unaobadilika kulingana na hali ni wa muhimu katika mazingira ya mabadiliko endelevu ya jamii na ulimwenguni kote.

b) *Kuweka mwelekeo*
Kazi ya kwanza kabisa ya uongozi wowote ni kuweka kusudi na mwelekeo wa shirika. Maswali matatu ya mwongozo katika kuonyesha mwelekeo ni pamoja na: Tuko wapi? Tunaelekea wapi? Tutafikaje huko? Kama ilivyonenwa, "Kama hujui uendako, unaweza ukajikuta unaishia mahala kwingine." Kadri tunavyopitia mazingira, mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati unatoa mfumo wa kuchambua maswala yanayofaa.

c) *Kufanya maamuzi*
Mojawapo ya makujumu ya uongozi ni kufanya maamuzi sahihi. Ni muhimu kutambua na kutofautisha kati ya maamuzi ya kawaida ya kila siku, na maamuzi

[3] Ibid., 43-60.

nyeti ambayo kwa kawaida huwa ni machache lakini muhimu sana.

d) *Ufanisi katika utendaji*
Mashirika, yakiwemo ya Kikristo, hukumbwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali. Mpango wa kimkakati huwasaidia viongozi kuwa mawakala wa rasilimali zilizopo chini yao wakipanga namna bora ya kuzitumia kwa ufanisi licha ya uchache wake.

e) *Upya wa shirika*
Madhehebu au mashirika, kama binadamu, hupitia katika hali zinazo shabihiana kwa kiwango kikubwa katika hatua za ukuaji wake: kuzaliwa, ujana, utu uzima, ukomavu, kudumaa, uharibifu na kifo. Kwa hiyo, Mpango Mkakati ni nyenzo ya msingi katika kuhakikisha upya na uhai wa mashirika ya Kikristo.

f) *Umoja wa shirika*

Mpango mkakati unahamasisha umoja na ushirikiano katika kazi kama timu. Timu nzuri haitakuwa na mashindano dhidi yao wenyewe, bali watashirikiana katika malengo na kazi moja. Juhudi za kila mmoja katika timu zinapaswa kuratibiwa, oanishwa, wanatimu kusaidiana, na kujielekeza katika lengo la kutimiza makusudio yao ya pamoja kama timu.

Ushauri wa Saffold kama ulivyoowekwa hapo juu na historia fupi kama ilivyofafanuliwa katika sura ya kwanza ndio msingi wa kuandaa Mpango, Mkakati huu. PAG (T) inatamani kupata mabadiliko makubwa katika kipindi cha miaka kumi ijayo. Kuna shauku kubwa miongoni mwa viongozi katika ngazi zote na kwa washirika wa kawaida kuona kanisa la PAG (T) likipiga hatua nyingine kwa kadri Tanzania na hata dunia inavyobadilika kwa kasi zaidi.

Ikizingatiwa kuwa theluthi moja ya watanzania ina umri chini ya miaka 25, huduma kwa vijana inalazimu juhudi za kimakusudi. Vilevile, zaidi ya 37% ya watanzania wanaishi mijini tofauti na miaka 20 iliyopita ambapo idadi ilikuwa kama 15%[4].Kasi ya wananchi kuhama kutoka vijiji kwenda mijini haizuiliki. Licha ya kwamba sasa Tanzania ni nchi yenye uchumi wa kipato cha kati, hali miongoni mwa wananchi haitii moyo. Umaskini unazidi kuvuruga maisha ya wengi na kudumaza vipaji miongoni mwa kizazi kijacho cha viongozi. Mambo ya sasa ni halisi kwetu na yamekuja na matokeo mabaya na mazuri kwa pamoja. Ukuaji wa kiteknolojia, ikiwa ni pamoja na matumizi ya mitandao ya kijamii ni nguvu isiyokwepeka katika kizazi hiki. Haya yote yanahitaji uongozi ulio makini kupambanua, kubadilika, kuendana na mazingira bila kuathiri misingi ya injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Maandiko yanatukumbusha umuhimu wa kanuni hii na jinsi ilivyotumiwa na viongozi wa Agano la Kale ambao “walikuwa na elimu ya kujua mambo ya nyakati na walijua kilichowapasa Israeli kufanya” (I Nyak. 12:32).

*4. Ingham, Keneth and Adolfo c.”Tanzania” Encyclodia Britannica, Inc,17 mar,2020, www.britannica.com/place/Tanzania*

# SURA YA TANO

# MCHAKATO WA KUANDAA MPANGO MKAKATI HUU

## 5.1 Toleo la Kwanza

Toleo la kwanza lilitolewa na kusambazwa kwa wajumbe wa Kamati ya Halmashauri Kuu ya PAG (T) kuipitia na kutoa maoni yao. Utafiti ulifanywa kwa viongozi wa Kanisa walioteuliwa. Toleo la kwanza pia lilifanya tathmini ya dhehebu (SWOT) na kutengeneza malengo na mikakati. Hata hivyo, baadhi ya takwimu za msingi na muhimu, na namna ya utekelezaji havikuwemo katika toleo la kwanza.

## 5.2 Toleo la Pili

Toleo la pili limetokana na marekebisho ya lile la kwanza. Baada ya kupokea maoni yao, Askofu Mkuu aliunda timu ya watu watatu kuyachambua na kuyajumuisha kwa pamoja na mengine ya awali. Wahusika walifanya utafiti mwingine kwa kutumia jukwaa liitwalo *Monkey Survey,* ili kupanua wigo wa mawazo na maoni kutoka kwa viongozi zaidi wa PAG (T). Viongozi sabini walichaguliwa bila kufuata utaratibu maalumu kama sampuli, wakiwemo maaskofu, waangalizi, wakurugenzi wa idara za vijana na wanawake, na wachungaji. Kati ya 70, viongozi 27 (sawa na 38.5%) waliitikia na waliosalia hawakuitikia. Kwa kuwa utafiti huu ulifanyika kimtandao, ilidhaniwa kuwa sababu ya wengi kushindwa kushiriki ni kutokana na wengi wao kutokuwa na kompyuta japokuwa wanazo simu za smatfoni. Hivyo, haikuwa rahisi kwao kutoa majibu kwa maswali yaliyohitaji maelezo kwa kutumia simu. Baada ya kupokea majibu kutoka kwa wale walioshiriki, timu ndogo ilikutana kuchambua taarifa kwa kuzingatia dira, dhima na maadili ya msingi, na tathmini ya ndani na nje (SWOT na PESTEL). Uchambuzi wa SWOT kutoka tolea la kwanza ulisaidia katika uchambuzi wa SWOT wa toleo la pili.

5.3 Warsha ya Mpango Mkakati

Kuhakikisha kuna uelewa wa pamoja miongoni mwa viongozi, warsha ya siku nne ilifanyika Dodoma kutoka Septemba 21-26, 2020 ambapo jumla ya viongozi wa juu 15 wa dhehebu walihudhuria. Hii ilihusisha Kamati Tendaji, viongozi wanne wa Idara wa kitaifa, Maaskofu wa Majimbo wawili na Waalikwa watatu waliowakilisha vijana na wasomi. Siku moja kati ya siku nne ilitumika katika maombi na kufunga. Kwenye hii warsha maeneo makuu ya Mpango Mkakati yalianishwa na kukubaliwa.

5.4 Timu ya Mpango Mkakati

Kwenye hitimisho la warsha iliyotajwa hapo juu, timu ndogo ya watengeneza Mpango Mkakati liliundwa kuendelea na kazi iliyobaki. Timu hiyo ilikuwa na wataalamu kama vile viongozi wa idara wa kitaifa, mwakilishi kutoka PAOC, wawakilishi wa vijana na mwakilishi wa elimu aliyeokoka kutoka serikalini. Timu hiyo ilifanya warsha ya wiki moja huko Zanzibar, Novemba 9-14, 2020 kwa ajili kuunda Malengo Mkakati na warsha nyingine huko Mwanza kutoka Januari 26-29, 2021 kwa ajili ya kuunda Mikakati, Shughuli na kumalizia kazi yote.

# SURA YA SITA

# UCHAMBUZI WA KIMAZINGIRA

6.1 Uchambuzi wa SWOT: Ndani

| NDANI | NGUVU | MADHAIFU |
|---|---|---|
| | a) Uwepo wa Chuo cha Biblia kinachomilikiwa na PAG (T) kiitwacho Mwanza Christian College na Shule za Biblia za Mikoa (RBS) ambazo huwaandaa viongozi wa kanisa la PAG (T) na madhehebu mengine.<br>b) Mtandao wa makanisa ya PAG (T) katika mikoa mingi ya Tanzania Bara na Zanzibar husaidia kuenea kwa kanisa katika maeneo ambayo bado hatujafika.<br>c) Idadi kubwa ya washirika wa dhehebu la PAG (T) ambao ni mtaji wa kijamii na rasilimali watu kwa ukuaji na upanuzi wa Kanisa<br>d) Tunao wachungaji wengi walio na elimu ya | a) Mtazamo wa kimasikini kwa baadhi ya washirika na viongozi umepelekea tatizo sugu la akili ya utegemezi.<br>b) Makanisa mengi yalianzia vijijini na kusambaa kuelekea mijini na majiji na hivyo kuchelewesha kazi maeneo ya mijini ambayo ingeliwezesha kanisa kifedha.<br>c) Kanisa la PAG (T) halikujighulisha na mahitaji ya kimwili na kijamii na kukosa umuhimu kijamii.<br>d) Hapajakuwepo na takwimu sahihi zilizoandaliwa na kutolewa jambo ambalo ni kikwazo katika kufanya tathmini ya maendeleo ya kanisa<br>e) Hakuna mpango wa pamoja katika kazi ya umisheni na uinjilisiti kuanzia ngazi ya kitaifa hadi kanisa la mahali.<br>f) Hakuna kujali katika |

| | | |
|---|---|---|
| | kitheolojia kwa viwango mbalimabli, kuanzia cheti hadi shahada ya uzamivu ambayo ni msingi mzuri wa rasilimali watu.<br>e) Tunamiliki viwanja vikubwa katika maeneo mengi ya mijini ambayo ni msaada mkubwa kwa huduma za mijini.<br>f) Washirika wa makanisa ya PAG (T) ambao wanafanya kazi katika mashirika mbali mbali ya kimaendeleo na serikalini. Uzoefu na pesa zao vyaweza kuwa msaada kwa kanisa.<br>g) Umoja na amani baina ya wana PAG (T), tofauti na miaka michache iliyopita, husaidia kupanga mipango ya muda mrefu na mfupi inayotekelezeka.<br>h) Katiba mpya ya PAG (T) inafungua milango mipya na kujenga mazingira rafiki kwa | utendaji hivyo kupelekea kufanya kazi kwa mazoea na hivyo kukwamisha maendeleo.<br>g) Utendaji wa idara zote za PAG (T), hasa idara ya watoto hauridhishi. Idara zote zinahitaji kuhuishwa na kuhakikisha zinasimama na kusonga mbele kulingana na mahitaji na majira yetu.<br>h) Ujuzi mdogo kwa uongozi wa shirika (utawala dhidi ya uongozi, mipango mizuri, ujuzi wa kawaida na maalumu) kwa baadhi ya viongozi wa PAG (T) hukwamisha mipango ya muda mrefu ya utekelezaji wake.<br>i) Uduni wa vielelezo, mifano, na programu za malezi na maandalizi (*mentorship*) kwa viongozi wachanga wanaoibuka kama viongozi wa kizazi kijacho.<br>j) Mfumo wa uwajibikaji usiotosheleza huchochea kutoheshimu na kupuuza au kutotii maelekezo ya viongozi.<br>k) Uelewa usio sahihi wa miradi ya maendeleo na haki za jamii na hivyo |

| | | |
|---|---|---|
| | mabadiliko endelevu. | kuathiri ujumbe wetu wa injili kukosa kugusa mambo hayo.<br>l) Matumizi haba ya vyombo vya habari na hasa mitandao ya kijamii.<br>m) Historia sugu ya utegemezi ambapo wachungaji wengi wana kumbukumbu za misaada na mitumba waliyokuwa wakipokea toka kwa wamishenari wa Kigeni. Hali hii inakwamisha juhudi za kupata kutafuta vyanzo vya mapato ya hapa nchini. |

| | FURSA | TISHIO |
|---|---|---|
| **NJE** | a) Amani na usalama nchini Tanzania inatoa fursa kutimiza Agizo Kuu na Amri Kuu.<br>b) Ushirikiano unaoendelea baina ya PAG (T) na PAOC, PAG (T) na CIT kama wabia muhimu katika kazi ya umisheni na vita dhidi ya umasikini miongoni mwa | a) Mafundisho potofu (injili ya mafanikio isiyo na uwiano, matumizi ya vitu kama maji, chumvi, udongo, mafuta, n.k., kwa ajili ya baraka na ulinzi) yanavutia makundi na hata kuwatega waamini wa kweli kunasika kwenye upotofu kama huo.<br>b) Matatizo yanayohusiana na umasikini kote vijijini na mijini na kusababisha changamoto mbali mbali |

| | | |
|---|---|---|
| | watoto na makundi yaishiyo katika mazingira hatarishi.<br>c) Serikali kutekeleza mikakati mbalimbali ya maendeleo na kupunguza umasikini kama vile TASAF, SDGs, TDV 2025, NSGRP/ MKUKUTA inatoa fursa zaidi kwa PAG (T) kuendeleza pale juhudi za serikali zinapoishia.<br>d) Uwepo wa vyuo vikuu na kati ni uwanja wa umisheni kwa kanisa katika kuwaandaa vijana kuwa viongozi bora wajao kwa ajili ya taifa na kanisa.<br>e) Uhuru wa kuabudu uliopo nchini ni faida kwa kanisa kuendeleza mikutano ya injili na makongamano kumvunia Kristo roho za watu.<br>f) Uwepo wa vyombo vya umoja wa Kikristo kama vile CPCT, CCT, TEC na | ikiwa ni pamoja na uhaba wa rasilimali kwa ajili ya majukumu ya kimisheni.<br>c) Utamaduni wa kuminya maoni binafsi na uhuru wa kujieleza husababisha watu wasitoe mawazo yao kwa uhuru na inaweza kupelekea kuua ubunifu na uvumbuzi.<br>d) Kupinga mabadiliko kutokana na ukosefu wa uelewa na desturi ya kulindana kama zao la itikadi za kijamaa hupelekea kurudisha maendeleo nyuma.<br>e) Athari za mabadiliko ya tabianchi husababisha matatizo kwa wakulima na maisha yao na hivyo kuathiri kanisa moja kwa moja.<br>f) Mtandao mbaya wa barabara katika baadhi ya maeneo hapa nchini ni kikwazo katika kueneza injili.<br>g) Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana ni tishio sio tu kwa kanisa bali kwa taifa pia uwezekano wa |

| | | |
|---|---|---|
| | SDA ambayo hutumika kupaza sauti za kitume na kinabii kwa niaba ya waamini wa Tanzania.<br>g) Upatikanaji wa ardhi na unafuu wa bei hapa nchini ni fursa kubwa kwa kanisa la PAG (T) kununua ardhi kubwa kwa ajili ya maendeleo na upanuzi wa siku zijazo.<br>h) Kukua kwa teknolojia – ikiwa ni pamoja na matumizi mapana ya mitandao ya kijamii, machapisho, na vyombo vingine vya habari kwa kielektroniki (runinga, redio, n.k.) havijatumiwa ipasavyo kama chachu ya maendeleo ya kanisa (mfano kuhubiri na kufundisha neno la Mungu kupitia redio na runinga). | mmomonyoko wa maadili. |

6.2 Uchambuzi wa PESTEL[4]: Nje

| Sababu za Kisiasa | Sababu za Kiuchumi |
|---|---|
